Azimio la pili la Norwich juu ya haki na usawa wa kimazingra

Kutoka kwenye kuzingatia kinga na tahadhari kuelekea kwenye kujumuisha haki za jamii husika: Utawala wa kidemokrasia wa misitu kama nyenzo kuu ya MKUHUMI wa usawa na wenye ufanisi.

Photography by: Adrian Martin

Sisi, ambao ni kikundi cha kimaifa cha wanaharakati, wana-taaluma, na watafiti, tunangamua kwamba ukosefu wa usawa uliokithiri unazidi kuathiri usimamizi wa misitu katika upande wa kusini mwa dunia.

Michakato ya kinga na taadhari za mkuhumi ambayo imeamzishwa chini ya mfumo wa umoja wa mataifa wa mabadiliko ya tabia nchi inatoa mwelekeo mpya katika kukabiliana na changamoto hizi.

Hata hivyo, michango mingi ya kinga na tahadhari hizi imeshindwa kushirikisha wananchi asilia na wananchi wengine wa kawaidia kwa namna stahiki kutokana na ukosefu wa uwazi pamoja na matumizi ya njia za kitaaliuma.

Tunaamini kwamba mkuhumi ambayo ya usawa na yenye ufanisi inaweza tu kupatikana endapo tutaachana na utaratibu juu-chini pamoja na utaratibu maalumu wa mchakato wa kinga na tahadhari ili kulete michakato hai ya kuimarishua usimamizi wa jamii wa maeneo ya misitu.

Tukisisitiza kwamba:
MKUHUMI hauwezi kuwa mfumo wa Nchi zenye viwanda kuhamishia wajibu wao wa kudhibi vyanzo vya mabadiliko ya nchi kwa nchi zinazoendelea, na kwamba kanuni ya wajibu wa pamoja kulingana na uwezo wa washirika, inasistiza mabadiliko kuelekea matumizi ya teknolojia zinazozalisha kiasi kidogo cha gesi joto katika katika nchi zilizoendelea;

Tukitambua kwamba
usimamizi uliopita na ule wa sasa wa misitu katika nchi zinazoendelea umezinyanganya jamii asilia na watu za kawaida rasilimali ardhi pamoja na misitu, na kuwatenga na maamuzi ya pamoja yanayohusiana na misitu na pia kudhohofisha mila, desturi na tamaduni zao;

Tunakubali kwamba
kutoshirikishwa kwa jamii asilia pamoja na jamii za kawaida imekuwa ndio chanzo kikubwa cha mifarakano katika misitu kwa vile serikali zimeshindwa kusikiliza matakwa ya waathirika kwa kuzingatia haki zao za kiuchumi, kisiasa, na kiutamadini; politiques et culturels;

Photography by: Poshendra Satyal

Tukizingatia kwamba
umiliki wa serikali wa rasilimali na sera za maendeleo zimekuwa ndio kiini cha uharibifu wa misitu na ukosefu wa usimamizi endelevu wa misitu;

Tunaguswa na ukweli kwamba
mwenendo wa dunia wa ubinafsishaji wa maeneo makubwa ya maliasili na uwezekano kwamba MKUHUMI inaweza kukuza mwenendo huu na hivyo kuongeza vikwazo vya usimamizi wa misitu miongoni mwa jamii husika;

Tunasisitiza kwamba
haki na usawa katika misitu ni pamoja na kukubali mapungufu yaliyopita na kuzuia mapungufu zaidi katika siku za usoni kwa njia ya kutambua na kuimarisha haki za jamiii asilia pamoja na jamii za kawaida, pamoja na maarifa na mifumo ya utawala.

Tunatambua kwamba
haki za jamii asilia na jamii za kawaida zimepiga hatua kubwa wa kipindi cha miongo miwili iliyopita, hasa kupitia utambuzi wa haki za makazi na sheria za kimila;

Kwa kuzingatia madhara halisi ya MKUHUMI
kwa jamii asilia na jamii nyinginezo pamoja na uwezekano wa shughuri za MKUHUMI kubadilisha migogoro inayohusiana na misitu na kusaidia kuleta usimamizi bora wa misitu.

Tukiwa tumeguswa na Ukweli kwamba
michakato ya sasa ya kinga na tahadhari za MKUHUMI zinaendelea kuwa hafifu hasa katika katka kujumuishwa katika maandalizi na utekelezaji wa shughuri za MKUHUMI;

Tukiwa tumefadhaishwa na ukweli kwamba
taratibu zilizopo za kisheria na za hiari kuhusiana na kinga na tahadhari za MKUHUMI zinapendelea zaidi mambo ya kitaaluma na hivyo kudhoofisha uwazi na uwezo wa wadau walio wengi katika kushiriki kwenye michakato ya MKUHUMI.

Tunasisitiza kwamba mitizamo hii ya umoja na uhalisia juu ya haki bado haijazingatiwa vya kutosha katika michakato iliyopo ya tahadhari na kinga za MKUHUMI katika ngazi za kidunia na kitaifa.

Photography by: David Mwayafu

Tunasisitiza
kwamba madai ya jamii asilia pamoja na jamii za kawaida juu ya haki na usawa kuhusiana na misitu yaangaliwe kwa mapana na mukitadha husika, sio tu kuhusu usawa katika ugawanaji wa mapato na majukumu bali pia katika utambuzi wa utamaduni na tofauti za watu, na maono ya wanajamii pamoja na uzoefu katika uhifadhi wa misitu na kushiriki katika taratibu za kidemokrasia za usimamizi wa misitu.

Tunasisitiza
kwamba mitizamo hii ya umoja na uhalisia juu ya haki bado haijazingatiwa vya kutosha katika michakato iliyopo ya tahadhari na kinga za MKUHUMI katika ngazi za kidunia na kitaifa. Michakato ya sasa ya kinga za MKUHUMI inahamasisha zaidi juu ya uwazi katika usimamizi wa misitu, kutambua na kuthamini ujuzi na haki za jamii asilia na jamii nyinginezo, pamoja na ushirikishwaji wa wadau katika shughuri za MKUHUMI.

Hata hivyo, tunatambua sababu zifuatazo ambazo ni kama ufafanuzi juu ya kushindwa kwa michakato ya sasa katka kutatua matatizo ya kihistoria ya ukosefu wa haki za kimisitu.

(1) Michakato ya sasa ya kinga inashindwa kuelezea umuhimu wa kutambua haki za kimazingira na kimira za jamii asilia na jamii za kawaida pamoja na madhara yake katika kuhifadhi misitu na usimamizi shirikishi wa misitu na ardhi za misitu.

(2) Michakato ya sasa inashindwa kuziwesha jamii asilia na jamii za kawaida kushiriki katika MKUHUMI kutokana na ukosefu wa uwazi, kutawaliwa na taratibu za kitaaluma pamoja na ukosefu wa mifumo ya kushughurikia manunguniko pamoja na ukosefu wa taratibu za uwezeshaji.

(3) Mifumo ya taarifa na viashiria vya kinga na tahadhari ni muhimu pale tu vinapoweza kusaidia jamii asilia na jamii nyinginezo kushiriki kikamilifu katika michakato ya MKUHUMI.

(4) Hii inahitaji mabadiliko katika msisitizo,kutoka kwenye utaratibu wa kinga na tahadhari zinazotoka juu kwenda chini na badala yake kuimarisha utawala wa kijamii ikiambatana na jitihada ambazo zinasaidia kurejesha na kutambua umuhimu wa mila, kutambua sharia za kimila pamoja na taasisi kwa ajili ya usimamizi wa maliasili pamoja na taratibu ambazo zinaboresha uwazi katika mchakato wa kinga na tahadhari na hivyo kuboresha ufikiwaji wa mfumo wa kutoa na kushughurikia malalamiko ya wadau.

Photography by: Cam Hoang

Kwa hiyo

tunasisitiza kwamba kuimarisha mifumo ya jamii ya usimamizi,ikiwa ni pamoja na utambuzi wa haki za kimazingira na sheria za kimiia ni kigezo muhimu sana katika kuandaa mfumo wa MKUHUMI ambao ni wa haki na ufanisi.

Tunapenda kuonyesha uungaji mkono wetu

kwa jitihada za kidunia juu ya haki za misitu pamoja na jitihada za jamii asilia pamoja na jamii nyingine katika kutaka kufikia usawa:

Tunaomba kwamba

mfumo wa Umoja wa mataifa wa mabadiliko ya tabia nchi uchukue jukumu la hiari na dhati la kusambaza vipengele muhimu vya 'Taarifa za mataifa' (national communications) kwa wadau walio wengi,na kuwezesha ufuatiliaji binafsi wa taarifa hizo kwa ajili ya kuazisha mifumo ya malalamiko juu ya MKUHUMI ili kushughurikia lawama ambazo hazipokelewi na kushughurikiwa vizuri na mamlaka husika katika nchi wanachama;

Tunasisitiza kwamba

serikali husika zianzishe mifumo ya wadau wengi kwa ajili ya kuboresha utawala wa kijamii kwa kujumuisha wawakilishi kutoka katika asasi za kijamii, jamii asilia na jamii za kawaida, kuanzisha mifumo ya malalamiko ya MKUHUMI pamoja na kusambaza taarifa za MKUHUMI katika namna ambayo ni muhafaka kwa wadau wote;

Msaada kwa wanaharakati na jitihada za haki za misitu

unahitaji utambuzi wa haki za kimazingira na sheria za kimila pamoja na bidii zao katika kuwakilisha jamii asilia na jamii za kawaida katika michakato ya kinga na tahadhari katika ngazi za kitaifa na kimataifa;

Tunahamasisha asasi za kiraia

kuongeza bidii katika kuboresha utawala wa kijamii pamoja na kufanya ufuatiliaji binafsi wa taaira za kitaifa zinazoenda kwa UNFCC, uperembaji wa shughuri za wafadhili na taasisi zao na kuandaa mitandao baina ya asasi na mashirika ambayo yanashughurika kwa ukaribu zaidi maswala haya katika nchi zinazoendelea;

Tunawasihi wafadhili wa kimataifa

kuheshimu na kusaidia kazi za mfumo wa wadau wengi katika kuandaa na kutekeleza miradi ya MKUHUMI, kufadhili mahitaji ya ujengaji uwezo kwa wawakilishi wa jamii asilia na jamii za kawaida pamoja na kutoa msaada wa kiufundi na kifedha katika kuboresha mifumo ya kijamii ya utawala, ikiwa ni pamoja na utambuzi wa haki za kimazingira na sheria za kimila;

Tunasisitiza kwamba Jitihadi za MKUHUMI ambazo zinashirikisha wadau walio wenge

kama vile Mfuko wa Ushirika wa Kaboni ya Misitu na Mradi wa Umoja wa Mataifa wa MKUHUMI, zisaidie ushirikishwaji wa usawa wa wawakilishi wa jamii asilia na jamii za kawaida na asasi za kiraiaka katika kuanzisha mifumo ya malalamiko katika ngazi za mtaa, taifa na kimataifa na katika uandaaji na utekelezaji wa mipango kwa kutambua haki za kimazingira na sheria za kimila za jamii asilia na jamii za kawaida.

WALIIOTIA SAINI:

Horacio Almanza Alcalde,
Instituto Nacional de Antropología e Historia, Mexico

Hari Dhungana,
Southasia Institute of Advanced Studies, Nepal

David Gritten,
Researcher

Nicole Gross-Camp,
University of East Anglia, UK

Esteban Gutierrez,
Instituto Venezolano de Investigaciones Científicas, Venezuela

Mirna Inturia,
Nur University, Bolivia

Cam Hoang,
Institute of Cultural Studies, Vietnam

Adrian Martin,
University of East Anglia, UK

Glory Massao,
Mpingo Conservation and Development Initiative, Tanzania

David Mwayafu,
Uganda Coalition for Sustainable Development, Uganda

Hao Phan,
University of East Anglia, UK

Iokiñe Rodríguez,
Instituto Venezolano de Investigaciones Científicas, Venezuela

Madhu Sarin,
independent analyst, India

Poshendra Satyal,
University of East Anglia, UK

Heike Schroeder,
University of East Anglia, UK

Thomas Sikor,
University of East Anglia, UK

Oliver Springate-Baginski,
University of East Anglia, UK

Global Environmental Justice Group, University of East Anglia
(www.uea.ac.uk/international-development/research/research-themes/environmental-justice)